JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

# Mbinu Bora za Kupunguza Mashambulizi ya Wadudu kwenye Viazi Vitamu



Kijitabu cha Mafunzo
Kwa Washauri wa Kilimo, Kanda ya Ziwa

1995

**Shukurani:**

- **Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ukiriguru**
- **Mradi wa Udhibiti Husishi Shinyanga (IPM)**
- **Farming Systems Project Lake Zone**

Kijitabu hiki kimetayarishwa na:

- Dr. M. Braun, IPM Shinyanga
- Bwana S.C. Jeremia, ARTI Ukiriguru
- Bwana J. Makula, IPM Shinyanga
- Mama C. Rugimbana, FSR Ukiriguru

Mchoraji wa picha: Bwana W.Temu

**Kwa msomaji:**

**Tunahitaji maoni yako kuhusu kitabu hiki**


1
AHAA! HILI TUTA LINA NYUFA ZITAKAZO RAHISISHA MAYAI YANGU KUINGIA


2
MIMI NATAGA MAYAI KWENYE HILI SHINA
NA MIMI NATAGA KWENYE HUU UFA WENYE KIAZI


3 FUNZA WANAKULA VIAZI
KUMBE MAMA YETU ANATUPENDA. TUMEZALIWA KWENYE CHAKULA KINGI HIVI.

4 MAMA KULWA ANAVUNA VIAZI




5
MUME WANGU, MSIMU HUU VIAZI VIMEHARIBIWA SANA NA WADUDU NITAVICHAMBUA VIBOVU VYOTE NITAWALISHA NG'OMBE
EEHE! KAPU LOTE HILO VIAZI VYOTE NI VIBOVU? KWA HIYO MWAKA HUU TUMELIMIA NG'OMBE


6
KAMA VIAZI VINAWEZA KUOZA KIASI HIKI, BASI HILI NI TATIZO SIJUI TUFANYE NINI?
TENA IMEKUWA NI BAHATI. HILI SWALI TUMUULIZE MTAALAM, HUYO ANAKUJA.


7
MTAALAM, HEBU ONA MAVUNO YA VIAZI YA MWAKA HUU.
LOO! WADUDU WAMEWAPA HASARA KUBWA. NAPASWA KUWAELEKEZA KANUNI BORA ZA KILIMO MTAKAPO ANZA KULIMA VIAZI TENA
TUTASHUKURU.


8
MAMA KULWA AMEANZA KULIMA TENA VIAZI MTAALAM ANAMWONYESHA JINSI YA KUCHAGUA MBEGU SAFI
WEWE MTAALAM! MBONA UNAACHA SEHEMU KUBWA YA RANDO INAYOFAA KUPANDWA?
HAPANA! NINAYOKATA NDIYO INAYOFAA. SEHEMU YA KATI NA YA NCHA MARA NYINGI HAINA WADUDU

9 USHAURI WA KILIMO CHA MZUNGUKO




10 BAADA YA WIKI NNE. PALIZI INAANZA
MTAALAM! NIMEANZA PALIZI.
NI SAWA, ILA UNAPOPALILIA JARIBU KURUDISHA UDONGO KWENYE TUTA ILI KUZIBA NYUFA KUZUIA WADUDU WASIINGIE KWENYE SHINA NA MIZIZI YA VIAZI


11
NYUFA KATIKA TUTA LA VIAZI KABLA YA KURUDISHIA UDONGO
BAADA YA KUZIBA NYUFA


12 PALIZI YA PILI BAADA YA WIKI NANE
TUMESHAURIWA KUWA, PALIZI YA WAKATI HUU IWE NYEPESI ILI TUSIHARIBU MARANDO. JEMBE DOGO AU MIKONO INAWEZA KUTUMIWA KUFUNIKA NYUFA.

# 13 KUVUNA KIDOGO KIDOGO



14 VIAZI HUWEZA KUANZA KUSHAMBULIWA NA WADUDU.



## 15 UTUNZAJI VIAZI KWA MATUMIZI YA BAADAYE



16 MAGANGA NA MKEWE MAMA KULWA WANAFURAHIA UTAMU WA VIAZI.

